maudhui yenye kuendekeza chuki	maudhui ambayo yanachochea au kuhamasisha mauaji ya kimbari au chuki dhidi ya kundi la watu linaloweza kutambulika;
hotuba ya chuki	hotuba ambayo, kwa maneno, sauti au picha au vinginevyo itakavyokuwa, ambayo inakebehi, kuharibu sifa, inachafua au inayoshusha sifa za mtu au kundi la watu kwa misingi ya rangi, mbari, dini, utaifa, jinsia, mwelekeo wa jinsi au ulemavu;

maudhui yasiyo na heshima	maudhui yoyote ambayo yanachukiza na kukera, yasiyofaa kimaadili na yanayokiuka viwango vya sasa na vinavyokubalika vya tabia njema; kama vile utupu na ngono.
Kibanda cha intaneti au kibanda cha mawasiliano mtandaoni	Sehemu inayotoa huduma za intaneti au kuwezesha watumiaji kujiunga na mitandao kwa kutumia kompyuta zake yenyewe au kompyuta makato za wateja; kwa kawaida kwa malipo;
chombo cha kusimamia sheria	Polisi, Idara ya Usalama wa Taifa, Mwendesha mashtaka au mamlaka yoyote iliyopewa nguvu kwa sheria yoyote iliyoandikwa;
maudhui machafu	maudhui ambayo yatafanya anayeyaona, kuyasoma au kuyasikia apate karaha kutokana na kuwepo kwa maandishi au picha za kiasherati na maudhui yenye mwelekeo wa uzinifu, ambayo hayana staha na ambayo yanaweza kuleta athari mbaya kwa wanaokutana nayo;
anayehifadhi maudhui mtandaoni (online content host)	kompyuta yoyote ambayo inahifadhi maudhui kutoka kompyuta nyingine iliyounganishwa kwenye mtandao; inayoweza kuhamisha taarifa kwenda kwa kompyuta nyingine iliyounganishwa kwenye mtandao; au inayowezesha maudhui yaliyo mtandaoni kufikiwa na watumiaji; ikiwa ni pamoja na mfumo wa kuhamisha taarifa kupitia kompyuta (file transfer protocol servers), kuunganisha kompyuta kubwa zilizo mbali (telnet servers), kampuni zinazohifadhi maudhui kwenye intaneti (webhosting companies) na kampuni kubwa zinazohifadhi maudhui ya intaneti (web servers);
mtandaoni	mfumo unaowezesha mazingira ya kupatikana kwa maudhui kupitia mtandao, ama kwa malipo au vinginevyo na ambayo yameanzia Tanzania au yamelengwa kutumiwa na umma Tanzania;
jukwaa la mtandaoni	majadiliano yanayofanyika kwenye sehemu maalum mtandaoni ambapo watu wanazungumza kupitia michango wanayotuma;
radio mtandao	huduma ya sauti; yenye leseni ya Mamlaka au la, ambayo inarushwa kupitia mitandao. Majina mengine ya huduma hii ni online radio, web radio, net radio, streaming radio, e-radio,au webcasting;
televisheni mtandao	usambazaji wa maudhui ya televisheni kidijitali, vipindi vifupi au video fupi vinavyotengenezwa na makampuni au watu mbalimbali; walio na leseni za Mamlaka na ambao hawana; na kusambazwa mtandaoni na ambayo yamelenwa kutumiwa Tanzania;
maudhui yasiyoruhusiwa	maudhui ambayo uchapishaji, usambazaji au uwekaji mitandaoni umekatazwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;
kitambulisho kinachotambulika	Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkazi, Leseni ya Udereva, Pasipoti na Kadi ya Mpiga Kura;
mitandao ya kijamii	mifumo ya mtandaoni iliyowekwa kwa msingi wa tekinolojia inayowezesha intaneti; ambayo inawezesha watumiaji kutunga na kubuni maudhui na kubadilishana na watumiaji wengine; hivyo kuwezesha watu binafsi, taasisi na jamiii kutumiana, kubuni kwa pamoja,kujadili na kurekebisha maudhui.
mtumiaji	mtu au taasisi ambao wanaweza kupata maudhui yaliyoko mtandaoni ama kwa kulipia au kwa utaratibu mwingine;
ukurasa wa tovuti au tovuti au 'saiti'	mafaili au maudhui ambayo yanapatikana kwenye mtandao wa kompyuta duniani, yaani www ambacho ni kifupisho cha World Wide Web; kwa kuandika anwani mahsusi ambayo inajulikana kama URL.
	Tanbihi: URL ni kifupisho cha Uniform Resource Locator; ambayo ni anwani ya ukurasa wa tovuti. Mfano wa URL ni https://www.tcra.go.tz/images/index.php/regulations ambapo www.tcra.go.tz ni mwenye tovuti na images/index.php/regulations ni sehemu ambako faili linapatikana.

Majukumu ya Wanaoweka maudhui mtandaoni

5. - (1) Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, mtoa huduma za maudhui mtandaoni atakuwa na majukumu kama ifuatavyo-

(a) kuhakikisha kwamba maudhui mtandaoni ni salama, yako katika hali ya usalama na hayakiuki matakwa ya sheria nyingine yoyote iliyoandikwa;

(b) kuweka maanani mwelekeo na hisia za kiutamaduni za umma kwa ujumla;

(c) kuweka sera au mwongozo kuhusu maudhui mtandaoni na kuwezesha kupatikana kwake kwa watumiaji;

(d) kutumia vifaa vya kusimamia na kuchuja maudhui yaliyokatazwa;

(e) kuweka utaratibu wa kutambua vyanzo vya maudhui;

(f) kuchukua hatua za kudhibiti maudhui yasiyotakiwa au yaliyokatazwa;

(g) kuhakikisha kwamba maudhui yaliyokatazwa yanaondolewa mtandaoni ndani ya saa kumi na mbili baada ya kutaarifiwa kufanya hivyo;

(2) Anayelipia shitariki na anayetumia maudhui mtandaoni atatakiwa kuzingatia yafuatayo:

(a) kuchukua dhamana na kuwajibika kwa mambo anayoweka mwenye majukwaa ya mtandaoni, mitandao ya kijamii, blogu au mifumo mingine mtandaoni inayofanana na hii;

(b) kuhakikisha kwamba mambo anayoweka mtandaoni hayakiuki matakwa ya Kanuni hizi au sheria nyingine.

(3) Mtoa huduma za maudhui mtandaoni atashirikiana na maafisa wa kusimamia sheria wakitekeleza majukumu yao chini ya Kanuni hizi.

Wenye leseni zinazoruhusu utoaji wa huduma kama vile internet, kupiga simu kupitia internet, takwimu kwa ajili ya biashara, na huduma za kutuma taarifa fupi

6. - (1) Mwenye leseni ya kutoa huduma mtandaoni anapoingia mkataba na watumiaji ataweka vigezo na masharti ambavyo, pamoja na mambo mengine, vitakuwa haki ya:

(a) kumkatalia mtumiaji huduma au kukatisha huduma kwa mtumiaji pale mtumiaji anapokiuka Kanuni hizi;

(b) kuondoa maudhui yaliyokatazwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Vigezo na masharti vitakavyowekwa ndani ya kanuni ndogo ya (1) vitakuwa katika namna na mfumo ambao utawawezesha watumiaji kuvipata kwa urahisi;

(3) Pale ambapo mwenye leseni atataarifiwa na Mamlaka au na mtu ambaye ameathirika na kuwepo kwa maudhui yaliyokatazwa; mwenye leseni atatakiwa, ndani ya saa kumi na mbili tangu alipopata taarifa ya Mamlaka, kumwelekeza mteja wake kuondoa maudhui hayo yaliyokatazwa;

(4) Baada ya kupokea taarifa chini ya kifungu kidogo (3), mteja atatakiwa, ndani ya saa kumi na mbili kuanzia muda aliyopewa taarifa, kuondoa maudhui hayo yaliyokatazwa;

(5) Pale ambapo mteja atashindwa kuondoa maudhui hayo yaliyokatazwa ndani ya saa kumi na mbili, mwenye leseni ataisimamisha au kuifungia akaunti ya mteja.

Mwenye blogu ya maudhui ya redio na televisheni mtandaoni

7. - (1) Mwenye leseni ya redio na televisheni mtandaoni vinavyotangaza kupitia intaneti kwa lengo na kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha umma atatakiwa kuzingatia masharti yafutayo:

(a) maudhui yatakayorushwa yatazingatia kanuni zinazotawala huduma za utangazaji;

(b) kuzingatia maadili ya uandishi wa habari na weledi;

(c) kulipa ada zinazotakiwa;

(d) kuwasilisha kwa msimamizi wa sekta mpango wa kuendeleza wafanyakazi wake;

(e) kuzingatia sheria na kanuni za haki ya kunakili na hakimiliki;

(f) kuzingatia masuala ya umilki na majukumu ya uendeshaji yaliyoainishwa kwenye Sheria;

(g) kuzingatia matakwa ya kuwa na maudhui yaliyoandaliwa Tanzania kwa mujibu wa kanuni.

(2) Kifungu kidogo (1) kitahusu Watanzania wakazi, raia wa Tanzania walioko nje ya nchi, watu wasio raia wa Tanzania wanaoishi nchini ambao wanaendesha blogu au majukwaa ya mtandaoni yenye maudhui yanayolenga kutumiwa na Watanzania.

(3) Muombaji wa leseni ya chombo cha habari mtandaoni chini ya kanuni hii atawasilisha maombi kwa Mamlaka na kutoa taarifa zifuatazo:

(a) anwani inayoeleza ilipo sehemu anapofanyia shughuli zake;

(b) hati ya usajili;

(c) mmilki na menejimenti ya mtandao;

(d) maelezo binafsi ya wafanyakazi kuhusu elimu, ujuzi (curriculum vitae);

(e) aina ya maudhui yatakayotolewa kama vile taarifa za habari, habari kwa ufupi na michezo (taarifa za vipindi);

(f) mwongozo na sera ya uhariri;

(g) saa za kazi;

(h) maelezo ya kitaalamu ya vifaa vinavyotumika;

(i) ufafanuzi iwapo ni huduma ya kibiashara au la.

Anayehifadhi maudhui mtandaoni (online content host)

8. Kwa kuzingatia Kanuni ya 5, anayehifadhi maudhui mtandaoni atatakiwa-

(a) kuwa na kanuni zenye masharti ya kuweka maudhui;

(b) atakapopata taarifa ya mtu ambaye ameathiriwa na

maudhui hayo au kutoka kwa Mamlaka au vyombo vya kusimamia sheria, ataondoa maudhui hayo aliyoweka.

Wanaotoa huduma za intaneti kwenye vibanda (internet cafes)

9. - (1) Kwa kuzingatia Kanuni 5, kila kibanda cha intaneti au sehemu ya biashara inayotoa huduma za intaneti atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuhakikisha kwamba kompyuta zote zinazotumiwa na wateja kwa huduma za intaneti zinawekewa utambulisho mahsusi ambao haubadiliki kwa kifaa husika(public static IP addresses);

(b) kutunga na kuchapisha sera ya matumizi salama ya intaneti kwa ajili ya matumizi salama ya intaneti kwa ajili ya maudhui mtandaoni na kuiweka mahali ambapo inaonekana kwa urahisi ndani ya sehemu huduma inapotolewa; au kwenye kioo cha kompyuta; au kuweka sera hiyo kwenye sehemu zinazoonekana ili watumiaji waisome kabla ya kutumia huduma hiyo;

(c) kuweka utaratibu wa kudhibiti watumiaji kupata maudhui yaliyokatazwa;

(d) kufunga kamera za kurekodi shghuli zote zinazofanyika ndani ya sehemu ya huduma za intanetina kuweka kumbukumbu ya picha ziizorekodiwa;

(e) kuweka na kutumia rejista ya kumbukumbu ya watumiaji wa huduma za intaneti na kuhakikisha kwamba kila mtu anayetumia huduma ya intaneti anasajiliwa baada ya kuonyesha kitambulisho kinachotambulika.

(2) Picha zitakazochukuliwa na kamera za kurekodi matukio na rejesta ya watumiaji kama ilivyoelezwa kwenye kifungu kidogo (1) vitahifadhiwa kwa kipindi cha miezi kumi na mbili.

Wanaotumia mitandao ya kijamii

10. Kwa kuzingatia Kanuni 5, mtumiaji wa mitandao ya kijamii atatakiwa:

(a) kuchukua dhamana na kuwajibika kwa taarifa atakazochapisha kwenye mitandao ya kijamii;

(b) kutumia neo la siri (password) kulinda vifaa anavyotumia au vinavyomuwezesha kutumia mitandao ya kijamii dhidi ya matumizi yasiyoidhinishwa, ama kutumiwa na mtu asiyeruhusiwa.

KUHUSU UTOAJI WA TAARIFA, MAUDHUI YALIYOKATAZWA NA KUWALINDA WATOTO

Utoaji wa taarifa

11. - (1) Mamlaka au mtu yeyoe aliyeajiriwa na Mamlaka hatatoa taarifa alizopewa au alizozipata wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kikazi kwa mujibu wa vipengele vya Kanuni hizi, ila tu pale ambapo taarifa hizo zinatakiwa na chombo chochote cha kusimamia sheria, mahakama au baraza lolote lililoundwa kisheria.

(2) Pamoja na kanuni ndogo ya (1) au vipengele vingine vya Kanuni hizi, mtu aliyeruhusiwa ambaye anatekeleza maelekezo au anajua kuhusu taarifa yoyote atazingatia yafuatayo-

(a) hatatoa taarifa hizo kwa mtu mwingine isipokuwa pale ambapo mtu huyo atakuwa afisa wa chombo cha kusimamia sheria na kwamba utoaji wa taarifa hizo ni muhimu kwa ajili ya kuwezesha utendaji kazi wa huyo mtu aliyeidhinishwa,au afisa wa kusimamia sheria ambaye anapokea taarifa hizo; au

(b) atatumia taarifa hizo kwa namna ambayo ni muhimu kwa utendaji wa kazi zake rasmi.

Maudhui yaliyokatazwa

12. Mtoa huduma za maudhui mtandaoni hatachapisha-

(a) maudhui yasiyofaa isipokuwa tu yake yaliyoidhnishwa na taasisi inayohusika na kuchuja filamu;

(b) maudhui machafu;

(c) hotuba za chuki;

(d) vitendo vya wazi vya ngono au ponografia;

(e) uhalifu unaohusisha ngono, ubakaji, kusudio la ubakaji, ngono isiyo na ridhaa ambayo ni jinai kisheria na ngono inayohusisha binadamu na wanyama;

(f) maudhui yanayoonyesha utumiaji nguvu, ama kwa vitendo, kwa maneno au kisaikolojia; na ambayo inaweza kutibua, kushtua na kuudhi watazamaji na kusababisha hofu kubwa miongoni mwa watazamaji au kuhimiza wengine kuiga matukio hayo;

(g) maudhui yanayoonyesha vitendo vya ukatili na utesi, kuumizwa, umwagaji wa damu na picha za watu wakiwa wanauawa waziwazi;

(h) maudhui yanayosababisha kero na maudhi, yanayotishia uharibifu au ubaya, yanayohimiza au kuchochea uhalifu; au ambayo yanaweza kusababisha vurugu katika jamii;

(i) maudhui ambayo yanatetea propaganda za chuki au ambayo yanahimiza mauaji ya kimbari au chuki dhidi ya kundi la watu linalojulikana;

(j) maudhui ambayo yanaweza kutishia usalama wa taifa au afya na usalama wa jamii, kama vile-

(i) kutoa maelekezo na mwongozo wa nanma ya kutengeneza mabomu, kuzalisha madawa ya kulevya au bidhaa feki;

(ii) kueneza taarifa za uwongo zinazohusu kuzuka kwa migogoro ya kimbari (racial tension);

(iii) vurugu katika sehemu fulani ya nchi;

(iv) kusambaza habari na taarifa zinazohusu uwezekano wa mashambulizi ya kigaidi;

(v) kusambaza au kuwezesha kupatikana kwa taarifa zinazohusu kuzuka kwa magonjwa hatari au ya kuambukiza;

(vi) maudhui yoyote yanayohusiana na masuala haya.

(k) maudhui yanayohusu lugha chafu ikwa ni pamoja

na- (i) matumizi ya maneno yanayoshusha hadhi ya mtu au ya matusi ambayo yanalenga kumuudhi mtu au kundi la watu;

(ii) matumizi ya maneno yasiyo na staha, katika lugha yoyote inayotumiwa na wengi katika Jamhuri ya Muungano, ambayo yanachukuliwa kuwa ni machafu, ikiwa ni pamoja na yanayotaja ngono au sehemu za siri;

(iii) hotuba za chuki.

(l) maudhui ya uwongo ambayo yanaweza kupotosha au kudanganya umma, isipokuwa tu kama imeelezwa awali kwamba maudhi hayo:-

(i) ni kejeli na maigizo ya kuchekesha;

(ii) ni ya kutunga;

(iii) yana maelezo ya awali kwamba maudhui sio ya kweli.

Kuwalinda watoto dhidi ya maudhui yasiyofaa mtandaoni

13. Mtu ambaye anatoa maudhui mtandaoni, anapata maudhui mtandaoni, anatunza au anatumia maudhui mtandaoni au anaendesha kibanda au sehemu ya kutoa huduma za intaneti atachukua hatua zote zinazowezekana kuhakikisha kwamba:

(a) watoto hawajisajili, hawapati au kuchangia maudhui yaliyokatazwa;

(b) watumiaji wanapewa utaratibu wa kuchuja maudhui na kusimamia maudhui kama wazazi.

UTOAJI WA LESENI

Wenye leseni zinazoruhusu utoaji wa huduma kama vile internet, kupiga simu kupitia internet, takwimu kwa ajili ya biashara, na huduma za kutuma taarifa fupi

14. - (1) Mtu yeyote ambaye anataka kutoa huduma za maudhui mtandaoni atajaza fomu ya maombi na kulipa ada kama ilivyowekwa kwenye kiambatanisho cha Kanuni hizi.

(2) Fomu ya maombi iliyotajwa kwenye kifungu kidogo (1) itaambatana na nyaraka na taarifa kama mamlaka itakavyohitaji.

Kufutwa kwa leseni ya huduma za maudhui mtandaoni

15. - (1) Mamlaka inayo haki ya kufuta leseni ya huduma za maudhui mtandaoni pale ambapo vigezo na masharti vimekiukwa.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), pale ambapo Mamlaka imaridhika kwamba mwenye leseni ya huduma za maudhui mtandaoni amekiuka au anakiuka Kanuni hizi au masharti ya leseni, Mamlaka itatoa notisi kwa maandishi ikitaka ukikukwaji huo urekebishwe ndani ya kipindi kitakachowekwa kwenye notisi hiyo.

Utaratibu wa watoa huduma za maudhui mtandaoni kushughulikia malalamiko

16. - (1) Mtu yeyote anaweza kuwasilisha malalamiko kwa mtoa huduma za maudhui mtandaoni dhidi ya watu walioelezwa kwenye Kanuni (2) kuhusiana na masuala yoyote yanayohusiana na maudhui yaliyokatazwa.

(2) Mtoa huduma za maudhui mtandaoni atatakiwa kutatua malalamiko yaliyowasilishwa chini ya Kanuni hii ndani ya saa kumi na mbili.

(3) Pale ambapo mtoa huduma za maudhui mtandaoni atashindwa kutatua malaamiko ndani ya muda uliowekwa chini ya kifungu kidogo cha 2, mlalamikaji anaweza, ndani ya siku 30 kuanzia siku aliyowasilisha malalamiko kwa mtoa huduma, kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka.

Kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka

17. - (1) Baada ya kupokea malalamiko chini ya Kanuni hizi, Mamlaka itampatia mtoa huduma nakala ya malalamiko na kumtaka mtoa huduma za maudhui mtandaoni kujibu ndani ya saa kumi na mbili.

(2) Pale ambapo mtu hajaridhika na majibu ya mtoa huduma za maudhui mtandaoni chini ya kifungu kidogo cha 1, Mamlaka inashughulikia malalamiko hayo kupitia utaratibu wa Kamati ya Maudhui.

Makosa na adhabu

18. Mtu yeyote ambaye atakiuka matakwa ya Kanuni hizi, anatenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi 12 au vyote.

ADA ZA LESENI ZA HUDUMA ZA MAUDHUI MTANDAONI (kwa shilingi)

Na.	Aina ya Leseni	Malipo ya maombi ya usajili	Ada ya kupatiwa Leseni	Ada ya Mwaka ya Leseni	Gharama ya Kuhuhisha Leseni (renewal)	Kipindi cha Leseni (miaka)
1	Blogu, Majukwaa mtandaoni	100,000	1,000,000	1,000,000	1,000,000	3
2	Televisheni mtandaoni	50,000	200,000	200,000	200,000	3
3	Radio mtandaoni	50,000	200,000	200,000	200,000	3

Taarifa zinazotakiwa unapoomba Leseni ya maudhui mtandaoni

Fomu za maombi ya leseni zinatolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania zinapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka, ambayo ni: www.tcra.go.tz. Ukishaingia, nenda kulikoandikwa *licensing*; shuka chini hadi *licensing information*; fungua *application forms*, kisha uone orodha ya fomu kisha ufungue unayoitaka.

Fomu iliyojazwa kikamilifu inatakiwa iwasilishwe ikiwa na taarifa na viambatanisho kama inavyoelezwa hapa.

A: Aina ya leseni inayoombwa

B: Taarifa za muombaji

1. Jina au majina ya muombaji:
Simu, fax, anwani ya barua pepe, tovuti, sehemu shughuli zinakofanyika (mji/jiji, mtaa, namba ya kwanja, postikodi.
2. Jina (majina) ya wenye hisa na idadi ya hisa zao kila mmoja.
3. Mtaji wa kampuni.
4. Uraia wa wenye hisa/wakurugenzi wa kampuni ya muombaji/
5. TIN na Tax Clearance Certificate.
6. Aina ya huduma zinazoombewa leseni (mfano, elimu, habari au burudani).
7. Eleza iwapo utatoa huduma maalum kama vile matukio na taarifa za habari.
8. Makisio ya gharama za uwekezaji.
9. Wafanyakazi wanaohitajika na elimu yao.
10. Mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi (kama upo).
11. Tarehe ambapo shughuli zinatarajiwa kuanza.
12. Mipango ya baadae.
13. Taarifa nyingine muhimu.
14. Jina, wadhifa wa anayesaini fomu.
15. Anayesaini atatoa tamko kwamba taarifa zote alizotoa kwenye fomu ni za kweli.
16. Muhuri rasmi wa kampuni.

(**Tanbihi:** Orodha ya postikodi kwa nchi nzima imechapishwa kwenye tovuti ya TCRA. Kwenye ukurasa wa kwanza, nenda palipoandikwa ***Postal Services***).

MAJIBU YA BAADHI YA MASWALI KUHUSU MAUDHUI MTANDAONI

Je, usajili huu unahusu pia Magrupu yanayotumia majukwaa/mitandao ya nje kama WhatsApp, Facebook, Instagram, n.k?

Usajili huu hauhusu watumiaji wa mitandao ya kijamii yenye wamiliki walioko nje ya nchi kama WhatsApp, Facebook, Instagram, n.k.
Hata hivyo, Kanuni ya 5, 7, 8 na 10 za Kanuni za Maudhui Mtandaoni (Online Content Regulations) za 2018, inawapa wajibu wa kutimiza watumiaji wote wa maudhui mitandaoni ikijumuisha wana-Group wote na Wasimamizi (Administrators) wake bila kujali unatumia majukwaa/ mitandao ya ndani au ya nje.

Je, wamiliki wa websites nao wanatakiwa kujisajili?

Hapana iwapo haijihusishi na upakiaji wa taarifa za mara kwa mara (Current News) vinginevyo itahitaji usajili.

Je, gharama za usajili ni kiasi gani?

Gharama za usajili zimefafanuliwa kwenye jedwali ukurasa za 24; na ni katika shilingi.

Je, wamiliki wa Radio na Televisheni walio na Leseni za TCRA kwa sasa lakini wanarusha pia matangazo yao kwa kutumia internet wanatakiwa kusajiliwa?

Ndiyo, TCRA ilitoa leseni moja tu ya kurusha maudhui ya matangazo kwa kutumia mitambo iliyosimikwa ardhini (Radio and Television Terrestrial services) na si vinginevyo

Je, usajili unafanyika kwenye mtandao pekee?

Ndiyo, fungua tovuti (website) ya TCRA (www.tcra.go.tz), upande wako wa kulia juu kuna maandishi yanasomeka (BROADCASTING) chini ya maandishi haya utaona linki yenye neno Online Content Services bofya na uendelee na usajili.

Muda wa Leseni ukoje?

Leseni zote ni za miaka mitatu ambapo baada ya muda huo itahitajika kuomba kuhuishwa na kupewa Leseni nyingine kwa anayekidhi vigezo husika.

MAUDHUI MTANDAONI YANAVYOSIMAMIWA NCHI NYINGINE

Nchi kadhaa zimeweka utaratibu wa kusimamia maudhui mtandaoni ambayo yanaelekwa kwa umma. Muhtasari huu unaelezea usimamizi huo nchini Uganda. Kenya, Malaysia, Australia, India, China, Falme za Kiarabu, Singapore, Uingereza na Marekani

Na	Nchi	Aina ya usimamizi	Maelezo
1	Uganda	1.Sheria ya kudhibiti ponografia (Anti-Pornography Act) ya mwaka 2014, 2. Taarifa kwa umma ilitolewa tarehe 6 Machi 2018 kwa mujibu wa Sheria ya matumizi mabaya ya Kompyuta ya 2011 Usajili wa watoa huduma za mawasiliano ya data na utangazaji	Inakataza ponografia kwa mfumo wowote ule ikiwa ni pamoja na mtandaoni Kulitolewa taarifa kwa umma wa mujibu wa kifungu 6(e) cha Sheria ya Mawasiliano Uganda ya mwaka 2013 ambayo iliwataka watu wote wanaotoa huduma za mawasiliano ya data mtandaoni (ikiwa ni pamoja na wachapishaji mtandaoni, majukwaa ya habari mtandaoni, waendeshaji wa redio na televisheni mtandaoni) kuomba na kupatiwa idhini kutoka kwa Tume ya Mawasiliano Uganda ifikapo 2 April 2018. Kuwaelekeza watoa huduma za intaneti (ISP) kuzuia upatikanaji wa tovuti au vyanzo vya maudhui haya.
2	Kenya	Sheria ya matumizi mabaya ya kompyuta na udhibiti wa makosa ya mtandao ya 2018	Kenya imepitisha, hivi karibuni, sheria ya matumizi mabaya ya kompyuta na udhibiti wa makosa ya mtandao ya Mei 2018. Ingawaje sheria haizungumzii moja kwa moja udhibiti wa maudhui mtandaoni, imeweka kipengele cha adhabu kwa maudhui na mambo yasiyotakiwa au yaliyozuiwa mtandaoni. Adhabu: Faini ya shilingi za Kenya milioni 5 hadi 25 na kifungo kati ya miaka 2 na 25.
3	Malaysia	Kanuni za Malaysia za mitandao na maudhui	Sehemu ya 5: Mwongozo mahsusi kwa mitandao. Kifungu 1.2 cha Kanuni kinahusu maeneo ambayo yanasimamiwa na kinawahusu watoa huduma za maudhui mtandaoni au wale wanaowezesha kupatikana kwa maudhui mtandaoni kwa kutumia tekinolojia zilizoko na ambazo zinakuja baadae. Hawa ni pamoja na: (a) Wanaotoa huduma za intaneti; (b) Wanaohifadhi maudhui ya intaneti kwa niaba ya wateja; (c) Wanaoandaa maudhui yanayopatikana kupitia intaneti; (d) Wanaowezesha kusambazwa maudhui ya intaneti (e) Wanaounganisha mitandao. Chini ya kifungu 99, Tume ya Mawasiliano inaweza kumuagiza mtu au kundi la watu, kwa mujibu kifungu cha 51 kuzingatia matakwa ya Kanuni hizi. Adhabu: Faini isiyozidi pesa za Malaysia (Ringit) 50,000 ambayo ni sawa na dola za Kimarekani (USD) 13,000).
4	Singapore	Sheria ya Utangazaji Taarifa kuhusu leseni ya jumla	a) mtu yeyoye aliyeko Singapore na ambaye anatoa vipindi; kwa madhumuni ya kibiashara, kisiasa au dini kwenye mtandao wa intaneti au b) taasisi au kikundi cha watu (ikiwa ni pamoja na chama chochote, biashara, klabu, kampuni, umoja, jamii, kikundi au ubia bila kujali kama vimeandikishwa chini ya sheria za Singapore au la) na ambavyo vinatoa vipindi vyovyote kwenye mtandao wa intaneti; ikiwa ni pamoja na wachapishaji mtandaoni na wanaohifadhi maudhui mtandaoni. Lazima waombe leseni ya kufanya shughuli hizi. Adhabu: Faini isiyozidi dola za Singapore ($) 30,000 au kifungo jela kwa kipindi kisichozidi miaka 3 au vyote.

Na	Nchi	Aina ya usimamizi	Maelezo
5	Australia	Sheria ya huduma za utangazaji ya 1992 Sheria ya Kuboresha usalama Mtandaoni, namba 24 ya 2015.	Sheria ya huduma za utangazaji ambao ilipitishwa 1992 inahusu usimamizi wa masuala kama vile utangazaji wa televisheni, masharti ya leseni na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Utangazaji Australia,ambayo sasa inaitwa Mamlaka ya Mawasiliano na Habari. Mwaka 1999 sheria ilirekebishwa na kuipa Mamlaka uwezo wa kusimamia maudhui mtandaoni Australia. Maudhui yaliyokatazwa yako chini ya Sheria ya Huduma za Utangazaji ya 1992 lakini usimamizi wa maudhui yaliyokatazwa uko chini ya Sheria ya Kuboresha usalama Mtandaoni, namba 24 ya 2015. Sheria hii imeanzisha ofisi inayoitwa Kamishna wa Usalama ambayo ina uwezo wa kutunga kanuni, kwa ajili ya kusimmia na kuhakiisha usalama mtandaoni Australia. Majukumu ya Kamishna ni pamoja na:- a) Kuendeleza usalama mtandaoni kwa watu wa Australia; b) Kushughulikia malalamiko yanayohsiana na maudhu mtandaoni; c) Kuratibu shughuli za Idara za Serikali kuu na wakala wanaoshughulika na usalama mtandaoni; d) Kusimamia masuala ya maudhui mtandaoni chini ya Sheria ya Huduma za Utangazaji; e) Kusajili watoa huduma za mitandao ya kijamii. Adhabu kwa kukiuka sheria ni kiwango sawa na dola za Kimarekani (USD) 15,500.
6	India	Kanuni za mitandao ya kijamii	Tarehe 6 April 2018 Wizara ya Habari na Utangazaji ya India iliagiza kuundwa kwa kamati ya watu 10 kubuni na kupendekeza mfumo wa usimamizi kwa ajili ya mitandao ya habari na taarifa ikiwa ni pamoja na watoa huduma za utangazaji wa kidijitali, watoa huduma za maudhui ya burudani, burudani na habari na wanaowezesha watoa huduma za habari na wenye mitandao ya kijamii kutoa huduma hizo. Hadidu za rejea za Kamati hiyo ni:- i. Kuainisha maeneo ya utoaji wa habari mtandaoni ambayo yanatakiwa kusimamiwa, kwa utaratibu unaotumika kwa magazeti na vyombo vya habari vya kielektroniki. ii. Kupendekeza utungaji sera unaofaa kwa ajili ya mitandao ya habari na taarifa na mitandao ya maudhui; ikiwa ni pamoja na utangazaj wa kidijitali unaojumuisha burudani, burudani na habari na wanaowezesha usambazaji wa huduma hizi mtandaoni; kwa kuzingatia kanuni, miongozo na miiko ya uandaaji na urushaji wa vipindi na matangazo ya kibiashara kwenye chaneli za televisheni. iii.Kufuatilia na kuchambua utaratibu wa kimataifa wa namna usimamizi wa masuala haya unavyofanywa kwa lengo la kuchukua mambo yaliyo bora.
7	China		Kuwezesha chombo cha China cha utawala wa mitandao kuwa chombo kinachowajibika na kuelekeza, kuendesha na kusimamia sheria kuhusiana na huduma za habari na taarifa kupitia mitandao nchini kote. Leseni inahitajika ili kutoa huduma za habari na taarifa kupitia intaneti. Hairuhusiwi kuanzisha shughuli za utoaji wa habari na taarifa kwa umma kupitia intaneti bila kuwa la leseni na kuzingatia matakwa na masharti ya leseni husika. Maombi ya leseni ya kutoa huduma za habari na taarifa kupitia intaneti yanatakiwa kukidhi masharti yafuatayo:- (1) Leseni iombwe na taasisi iliyoanzishwa kisheria ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Watu wa China; (2) Wahusika wakuu na mhariri mkuu wawe raia wa China;

Na.	Nchi	Aina ya usimamizi	Maelezo
	China		(3) Muombaji awe na wataalamu mahsusi wa kuhariri habari, wa kupitia maudhui na wenye ujuzi wa tekinolojia inayotumika kwa huduma hizo; (4) Muombaji awe na mfumo uliokamilika wa kusimamia huduma za habari na taarifa kupitia mtandao wa intaneti; (5) Kuwa na mfumo uliokamilika wa kusimamia usalama wa mitandao na mfumo wa kuhifadhi na kutunza mitandao inayotumika kutoa huduma hizo; (6) Kuwe na sehemu ya kufanyia shughuli na vifaa vinavyotakiwa na fedha za kuwezesha kutolewa kwa huduma hizo. Adhabu: Faini ya pesa za Kichina Yuan kati ya 10.000 (sawa na dola za Kimarekani (USD) 1,600 na 30.000 (USD 4,700).
8	Falme za Kiarabu (UAE)	Kanuni za mtandao ya kielektroniki,2018	Kanuni zinahusu mitandao yote ya kielektroniki inayoendeshwa kwenye Falme za Kiarabu (UAE). Shughuli zinazohusika zimelezwa kwenye Kanuni hizo kama ifuatavyo:- • Tovuti za kufanyia biashara; zinazotoa na kuuza maudhui yaliyoko kwenye mfumo wa sauti, video au machapisho; • Kutoa huduma za uchapishaji na uchapaji mtandaoni pale zinapotakiwa; • Tovuti maalum (utoaji wa matangazo ya kibiashara mtandaoni, tovuti za habari na kadhalika) na • Shughuli yoyote ya kielektroniki itakayoainishwa na msimamizi wa sekta. Ili kupata leseni ya kutoa huduma za habari mtandaoni, muombaji anatakiwa kujaza kikamilifu na kuwasilisha fomu ya maombi ya leseni (na fomu nyingine yoyote) kwa taasisi inayosimamia shughuli hizi. Anatakiwa kuambatanisha nyaraka muhimu na kulipa ada zinazotakiwa. Tarehe ya ukomo: Watoa huduma za habari mtandaoni waliopo wanatakiwa kupata leseni za utoaji wa habari mtandaoni ifikapo Juni 2018. Adhabu: Faini sio chini ya pesa za UAE Dirham 5,000 (sawa na dola za Kimarekani (USD) 1,400) au vinginevyo tovuti na mitandao yao ya kijamii vitafungiwa.
9	Uingereza	Mapendekezo ya kutunga Kanuni za Intaneti, 2017	Tarehe 26 Aprili 2016 Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May alitangaza hatua za Uingereza kusimamia intaneti. Wakati huo huo: Kuna vyombo viwili vya utoaji wa leseni ambavyo vinafaa kuangaliwa nchini Uingereza; ambavyo ni PRS na PPL. Iwapo mtu anataka kuendesha kituo cha redio mtandaoni ambacho kitacheza muziki kibiashara nchini Uingereza anatakiwa awe na leseni ya PPL na ya PRS ili shughuli zake zitambulike kisheria. Leseni hizi hazihitaji malipo ya ada ya kila mwezi au mahesabu ya mrahaba na badala yake zinalipiwa ada ya mwaka.
10	Marekani	Utoaji leseni kwa redio na televisheni mtandaoni	Ili kutoa matangazo ya redio mtandaoni Marekani, mhusika anatakiwa kuomba leseni iliyowekwa kisheria. Kuna vyombo vikuu vinne vinavyotoa leseni kisheria Marekani: • ASCAP (Chama cha watunzi wa nyimbo, waandishi wa vitabu na wachapishaji), • BMI (Taasisi inayosimamia muziki unaorushwa na vyombo vya utangazaji), • SESAC (Chama cha kusimamia haki za watunzi wa nyimbo na wachapishaji), • Sound Exchange (kinasimamia hakimiliki za wasanii). Taasisi tatu za mwanzo zinasimamia haki za watunzi na ya mwisho inasimamia haki za wasanii. TANBIHI: Ni vyema kutambua kwamba lengo la utoaji wa leseni kwa redio na televisheni mtandaoni limejikita kwenye kulinda haki za watunzi na kuhakikisha ukusanyaji wa mapato; na halihusu masuala ya maudhui.

TEHAMA na Changamoto Mitandaoni

William Shechambo
Barua pepe: willygs18@gmail.com

Ukuaji wa teknolojia na kuvumbuliwa kwa njia za kisasa katika sekta ya habari na mawasiliano kumerahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa njia ya simu za mkononi.

Simu imekuwa wakala mkubwa wa fedha ambapo kila wakati yupo karibu kumhudumia mteja kwenye kuhamisha fedha, kutuma, kutoa au hata kuweka.

Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Uwekezaji Ulaya (European Investment Bank, 2015) Afrika imeongoza duniani kwa matumizi ya simu za viganjani kufanya miamala ya kifedha.

Kikanda, hususan kwa Afrika Mashariki, Kenya ndio ilitajwa kuibuka kidedea kwa wakati huo ambapo wananchi 6 kati ya 10 (62%) ya watu wake wamekua wakitumia simu za viganjani kufanya miamala ya kifedha.

Mwaka 2017 Tanzania ilitikisa mno hasa kutokana na kupiga hatua kubwa kwenye huduma jumuishi za kifedha. Pamoja na mafanikio haya yote, ikiwemo ongezeko kubwa la watumiaji wa mtandao na miamala ya kifedha kwa simu za mkononi balaa lingine la uwepo wa matapeli liliibuka.

Kumekuwa na idadi kubwa ya watu wenye nia mbaya ambao hutumia maendeleo haya ya teknolojia kujipatia fedha kwa njia zisizo halali kutoka kwa watumiaji wa huduma za mtandao.

Licha ya matukio ya wizi wa fedha kwa njia ya mtandao kupungua nchini kwa sasa, ikilinganishwa na miaka iliyopita, wizi wa fedha kwa miamala ya simu umeonekana kushika kasi huku mkoa wa Dar es salaam ukiwa katika nafasi ya juu ukifuatiwa na Mwanza.

Taarifa na takwimu za matukio ya wizi wa mtandao zilizotolewa na Jeshi la Polisi, zinathibitisha kuwa kuanzia Oktoba 2016 hadi Machi 2017 mkoa wa Dar es salaam ulikuwa na matukio 1,423 ya wizi wa fedha kwa njia ya mtandao wa simu huku ukifuatiwa kwa mbali na mkoa wa Mwanza uliokuwa na matukio 659.

Mikoa mingine iliyotajwa kuwa na matukio mengi ya wizi wa fedha kwa njia ya simu ni Arusha, Dodoma, Morogoro na Mjini Magharibi (Zanzibar).

Kwa kipindi hicho kulikuwa na matukio 5,253 ya wizi wa fedha kwenye mtandao wa simu katika mikoa 19 ya Tanzania Bara na Visiwani. Matukio yaliyoripotiwa mkoa wa Dar es salaam ni sawa na asilimia 27 ya matukio yote. Katika mikoa mitatu ya Mwanza, Mjini Magharibi na Dodoma kulikuwa na matukio1,648.

Tofauti hiyo kubwa ya mkoa wa Dar Es salaam ikilinganishwa na mikoa mingine inatajwa kuchochewa na ongezeko la idadi ya watu wengi wanaotumia miamala ya simu kuliko taasisi nyingine za fedha zikiwemo benki.

Ndani ya mkoa wa Dar es salaam pia kuna tofauti kubwa kutoka wilaya moja hadi wilaya nyingine, kwa mfano, matkio yaliyoripotiwa wilaya ya Kinondoni yalikuwa 1,303 ikifuatiwa kwa mbali na wilaya ya Temeke (101) na Ilala (19).

Tofauti hii inaweza kuthibitisha kuwa tatizo la wizi wa fedha kwa njia ya mtandao wa simu ni kubwa zaidi katika wilaya ya Kinondoni kuliko maeneo mengine ya nchi. Inawezekana pia hii ni kutokana na ukubwa wa Kinondoni ambayo sasa imegawanywa na kuzaa Ubungo. Kinondoni pia ina wakazi wengi zaidi ya wilaya nyingine za Dar Es Salaam; 1,775,049 ukilinganisha na Ilala 1,220,611 na Temeke 1,368,881.

Pamoja na hilo, ni kwenye takwimu hizo hizo za Jeshi la Polisi, mikoa ya Geita, Tabora, Mtwara, Iringa, Tanga, Manyara na Kigoma ilitajwa kuwa na matukio machache ya uhalifu wa kifedha mitandaoni.

Kwa kipindi kati ya Mei 2017 na Mei mwaka huu, naamini kutokana na juhudi zilizofanywa na jeshi la polisi, wananchi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), takwimu hizi zitakuwa zimeshuka kwa kiasi kikubwa.

Sote tumeona namna ambavyo TCRA wanafanya kazi yao wakishirikiana na kitengo maalumu cha polisi cha halifu mtandaoni ambacho kikipelekewa shauri hulishughulikia haraka na wahalifu kunaswa. Hii ni kutokana na uwepo wa vifaa vya kisasa vya kiteknolojia ua uchunguzi wa uhalifu mtandaoni.

Kipekee niipongeze TCRA, na kampuni za simu nchini, kwa kuendelea kutoa elimu na tahadhari kwa watumiaji wa simu za mkononi kuwa makini na matapeli ambao hutumia ujumbe wa simu kujipatia fedha kwa udanganyifu.

Licha ya kushamiri kwa ujumbe wa kila aina kama vile, “amekubali, tuma hapa” au “mbona hujatuma ile fedha,” na nyingine nyingi tu; watu wamekuwa makini ambapo wanawabaini mapema sana matapeli hawa.

Penginepo duniani shirika linalofuatilia wizi katika mitandao (ACFE, the nationals on occupational fraud and abuse, 2016), linaeleza kuwa kesi 2,410 zimeripotiwa katika nchi 114 ambapo dola bilioni 6.3 zimepotea kutokana na wizi wa mtandao.

Kwa ukanda wa Afrika Mashariki, ripoti ya hivi karibuni inasema Kenya ndiyo inayoongoza kuwa na matukio mengi ya wizi wa mtandao kupitia simu ambapo kila mwaka kuna matukio ya kiasi cha shilingi bilioni tano (5) za Kenya na kiasi hicho kinaendelea

kuongezeka.

Umakini mkubwa unahitajika kwenye mtandao au tovuti inayouliza maelezo yoyote kati ya yafuatayo: majina ya mtumiaji, maneno siri (PIN), nambari za usalama wa jamii au Bima, nambari za akaunti ya benki na au siku yako ya kuzaliwa.

Mbali na hiyo, watumiaji wanashauriwa wasitume neno la siri kupitia barua pepe na kuwashirikisha watu wengine kwa sababu maneno hayo au namba ni ufunguo wa akaunti zako na huduma mtandaoni.

Kama ilivyo katika maisha nje ya mtandao, unapaswa kuwa mwangalifu na mtu unayempa funguo za mlango wa nyumba yako. Kwenye mtandao mambo ni hivyo hivyo; PIN ni kwa ajili yako tu, usimuamini mtu.

KUMBUKA

Tovuti na huduma halali, kamwe hazitakutaka uwatumie neno la siri au namba ya siri ya akaunti yako yoyote kupitia barua pepe, hivyo ukipata maombi ya namna hiyo usijibu, hao ni wezi.



TCRA imechapisha na inasambaza mwongozo maalum kwa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano; ambao, pamoja na maudhui mengine, una tahadhari anazotakiwa kuchukua mtumiaji ili kuepuka wizi na ulaghai mtandaoni. Pichani, Waziri wa Habari, Utamaduni, Michezo na Sanaa; Dr Harrison Mwakyembe, (katikati), Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashata Nditiye (wa pili kulia); Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Angelina Madete (wa pili kushoto); Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TCRA, Dr Jones Killimbe (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka, Mhandisi James Kilaba (kushoto) wakati wa uzinduzi wa mwongozo huo Dar Es Salaam mapema 2018.

Taarifa kwa Umma

UFAFANUZI JUU YA USAJILI WA WATUMIAJI WA MITANDAO YA KIJAMII KAMA FACEBOOK, INSTAGRAM NA TWITTER

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inauarifu umma kwamba:-

1. Wamiliki wote walio na leseni za utangazaji wanaotumia mitambo iliyosimikwa ardhini (Terrestrial) endapo watapenda kutumia pia kurasa za mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram na Twitter) kurusha maudhui yao (content streaming) kwa lengo la kuhabarisha umma ni lazima wajisajili kwanza TCRA.

2. Wamiliki wote wa Blogu, majukwaa mtandaoni (Online Forums), Redio na Televisheni mtandaoni ambao wamekuwa wakitoa huduma za maudhui mtandaoni kabla ya usajili kuanza, walizuiliwa kuhamishia huduma hizo kwenye Facebook, Instagram, Twitter na nyinginezo za kufanana na hizo.

3. Kwa watumiaji mmoja mmoja (individual users) wa mitandao hiyo ya kijamii hawahitaji kusajiliwa na TCRA isipokuwa Kanuni zinataka wawajibike kwa maudhui wanayoyapakia (uploading) kwenye mitandao hiyo.

Pamoja na kwamba TCRA itaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa watakaobainika kuhusika na upotoshaji huu, TCRA inavitahadharisha vyombo vya habari na watumiaji wa mitandao ya kubebea maudhui kujiepusha na usambazaji wa taarifa zisizokuwa na ukweli.

Kwa ufafanuzi au maelezo zaidi tumia barua pepe: onlinecontent@tcra.go.tz au Piga namba +255 22 2199769 au +255 22 2412011 wakati wa kazi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISO 9001:2015 CERTIFIED






Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania(TCRA) ni taasisi ya Serikali inayosimamia sekta ya mawasiliano. TCRA ilianzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania Na 12 ya 2003. TCRA ina viwango vya ISO 9001:2015.

Maeneo yanayosimamiwa

Mitandao ya simu na intaneti, masafa ya mawasiliano,huduma za Posta na usafirishaji wa vipeto katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huduma za utangazaji (kama vile redio na televisheni) kwa Tanzania Bara tu. Zanzibar ina Tume inayosimamia utangazaji.

Kazi za TCRA

- Kutoa leseni, kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni
- Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa
- Kuweka viwango vya kanuni na masharti ya kusambaza bidhaa na huduma zinazosimamiwa
- Kudhibiti viwango na bei
- Kufuatilia utendaji wa sekta ya mawasiliano kuhusiana na viwango vya uwekezaji; upatikanaji wa huduma, ubora na viwango vya huduma; gharama za huduma; ufanisi wa bidhaa na usambazaji wa huduma.
- Kufanikisha utatuzi wa malalamiko na migogoro baina ya watoa huduma na kati ya mtoa huduma na mtumiaji wa huduma.
- Kufanya kazi na kutekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa sheria husika
- Kusambaza taarifa kuhusu mambo ambayo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za Mamlaka.

TCRA na ustawi wa Watanzania

Katika kufanya kazi zake, Mamlaka inajitahidi kuendeleza ustawi wa jamii ya Tanzania kwa:-

- Kukuza ushindani unaofaa na ufanisi wa uchumi
- Kuendeleza upatikanaji wa huduma zilizodhibitiwa kwa watumiaji wote ikiwa ni pamoja na wenye kipato kidogo waliopo vijijini na wateja walio katika mazingira magumu.
- Kulinda maslahi ya watumiaji
- Kuendeleza elimu kwa wananchi kuhusu utambuzi na uelewa wa sekta zilizodhibitiwa ikiwa ni pamoja na haki na wajibu wa watumiaji;namna ambavyo malalamiko yanaweza kuwasilishwa na kutatuliwa na kuhusu majukumu, kazi na shughuli za Mamlaka.



Tanzania Communications Regulatory Authority

ISO 9001:2015 CERTIFIED

ZONAL OFFICES



Lake Zone
NSSF Commercial Complex,
4th Floor Wing B,
Kenyatta Road,
P. O. Box 3108,
33194 MWANZA.
Tel/Fax: +255 28 250 5081/2
E-mail: mwanza@tcra.go.tz

Northern Zone
Summit Centre, 3rd floor,
Block B
Sokoine Road,
P. O. Box 15675,
23194 ARUSHA
Tel +255 27 254 8947
E-mail: arusha@tcra.go.tz

Zanzibar Office,
19 Mbuyukisutu,
Chukwani Area,
P. O. Box 3284,
71194 ZANZIBAR
Tel/Fax: +255 24 223 5062,
E-mail: zanzibar@tcra.go.tz

Central Zone
LAPF Complex
SIDO AREA
P. O. Box 2229
41194 DODOMA
Tel: + 255 26 232 1731
+255 732 961 625
E-mail: dodoma@tcra.go.tz

Southern Highlands Zone
Century Plaza Building
1st Floor
Tunduma Road,
P. O. Box 1375,
51194 MBEYA.
Tel: +255 25 250 5016,
+255 25 252 5017,
E-mail: mbeya@tcra.go.tz

Eastern Zone
147 Kajenga Road,
Mikocheni,
P.O Box 35615
14194 Dar Es Salaam
E-mail: easternzone@tcra.go.tz